Kristo – Mwenye Mamlaka Mkuu Wa Kanisa

(Christ – The Supreme Head Of The Church)

Na

Ellis P. Forsman

Kristo – Mwenye Mamlaka Mkuu Wa Kanisa

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Kristo – Mwenye Mamlaka Mkuu Wa Kanisa

Efe. 1:

Efe. 1:22-23, "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole kiasi; juu ya mambo yanayofanana na hayo hakuna sheria."

Kol. 1:18, "Naye ndiye kichwa ya mwili yaani cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote."

Hakuna ukweli uliozoeleka zaidi katika Agano Jipya kuliko ukweli kwamba Yesu Kristo ndiye Mwenye Mamlaka Mkuu wa mwili wake, kanisa.

Kuna aina nyingi za maneno katika Agano Jipya inayoweza kutupa picha ya kanisa, na Kristo ni mkuu kwa kila mmoja wetu.

Kanisa ni ufalme

Mat. 16:16-19, "*Simoni Petro akajibu akasema, wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakwambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwambaa huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Naami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lo lote utakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.*"

Chini ya sitiari hii tunaona serikali ya baadae ya kanisa.

Kristo alilinunua kanisa kwa damu yake mwenyewe. Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunu kwa damu yake mwenyewe.*"

Wale aliowafungua kutoka dhambini kwa damu yake, amewafanya hawa kuwa ufalme wake.

Ufu. 1:5-6, "*Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu naye ni Baba yake utukufu una yeye hata milele na milele. Amina.*"

Kadiri Kristo alivyolinunua kanisa kwa damu yake mwenyewe, na wale aliowafungua kutoka dhaambini amewafanya kuwa ufalme; hivyo basi, ni wazi kwamba kanisa na ufalme ni mamoja.

Katika hotuba ya Petro siku ya Pentekoste alitangaza kwamba Mungu amemfufua Kristo kukaa katika kiti cha enzi cha Daudi. Mdo. 2:29-30, "*Waume ndugu zangu mniwie radhi niseme kwa ujariri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo. Basi kwa kuwa ni nabii akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi;*"

Hivyo, inafutia kwamba Kristo anakaa katika kiti cha enzi cha Daudi, au sivyo hajafufuliwa kutoka wafu.

Kinachofuata ni nini kama Kristo hakufufuliwa kutoka katika wafu? Imani yetu ni bure na tungali katika dhambi zetu. 1 Kor. 15:17, "*Na kama Kristo hakufufuka imani yetu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu.*"

Wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili ataacha kuwa mfalme, maana atakabidhi ufalme kwa Mungu. 1 Kor. 15:24-26, "*Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote na nguvu. Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.*"

Kanisa ni mwili

- 1 Kor. 12:27, "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja peke yake.*"
- Efe. 5:30, "*Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake.*"

Katika sitiari hii tunaona muonekano wa ushirika wa kanisa na mfumo mkuu wa umoja katika Agano Jipya.

Kama kulivyo na umoja katika mwili, ndivyo kunapaswa kuwa na umoja katika mwili wa Kristo, ambalo ni kanisa lake. Rum. 12:4-5, "*Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo kila mmoja kwa mwenzake.*"

Lakini kwa nini kuna muunganiko katika mwili? Kwa sababu kila kiungo cha mwili kina wajibika kwa kichwa na ni kichwa kimoja pekee.

Ikiwa wote wanaokiri kuwa ni viungo katika mwili wa Kristo wangemtambua Kristo kama mwenye mamlaka mkuu, kusinge kuwa na vitu kama madhehebu, tafrija, na migawanyiko.

Kristo hakufanywa kichwa cha kanisa hadi alipofufuliwa katika wafu. Kabla ya kifo chake alisema kwamba hawezi kufanya chochote yeye mwenyewe. Yohana 5:19, "*Mwana hawezi kutenda neno mwenyeweil lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye ndiyo ayatendayo Mwana vile vile.*"

Lakini baada ya kufufuka kwake alisema, Mat. 28:18, "*…Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*"

Lakini Kristo alifufuliwa katika wafu ili asife tena. Rum. 6:9, "*Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena.*"

Hivyo basi, Kristo hatakufa tena na amechukua nafasi yake kama Kichwa cha kanisa Lake kwa yeyote mwenye nyama.

Yesu ataendelea kuwa "*kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa.*" (Efe. 1:22), hadi atakapo kuja mara ya pili "*kumpa Baba ufalme.*" (1 Kor. 15: 24).

Hivyo basi, hatupaswi kuangalia kila mwenye mwili duniani kama kichwa cha kanisa, na kitengo chochote ambacho mwanamke au mwanaume ni kichwa haiwezekani ikawa kanisa la Kristo.

Kanisa ni hekalu

1 Kor. 3:16-17, "*Hamjui ya kuwa ninyi mmkuwa hekaalu la Mungu, nay a kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.*"

Hapa tunaona matukio ya ibada ya kanisa.

Kristo ndiye kuhani mkuu "juu ya nyumba ya Mungu."

- Ebr. 4:14, "*Basi iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu.*"
- Ebr. 10:21, "*Na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu.*"
- Kuwa kuhani wetu mkuu, ni kupitia yeye ndiyo tunamkaribia Mungu.
- Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ilaa kwa njia ya mimi.*"
- Ebr. 10:20, "*Njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani mwili wake.*"

Kwa vile ni kupia yeye kwamba ndio tunamfikia Baba, hakuna sehemu ya ibada yetu inayokubaliwa na Mungu kama isipofanywa kulingana na mamlaka yaa Kristo. Kol. 3:17, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*"

Kwa sababu hii makanisa ya Kristo kila mahali yanachukua tahadhari kubwa kuondoa kila kitu kaatika ibada amacho hatuwezi kupata "*asema Bwana*" katika Agano Jipya.

Hivyo basi, inapaswa kutusukuma tusimwabudu Mungu kama Nuhu alivyofanya wakati wa wazee, au kama waisraeli walivyofanya kipindi cha Wayahudi, lakini mfumo mzuri wa ibada yetu leo ni lile la kanisa la mitume ya karne ya kwanza ya wakati wa Wakristo.

Wakati kusanyiko la wakati ule walikusanyika kuabudu katika Siku ya Bwana, iligawanyika katika sehemu kuu tano za ibada, ambazo ni:

Kushiriki meza ya Bwana: Mdo. 20:7, "*Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutaana ili kuumega mkate, Paulo akawahututubu akiazimu kusafiri siku ya pili yake,..*"

Mahubiri: Mdo. 20:7 (hapo juu).

Kuchanga fedha: 1 Kor. 16:2, "*Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;*"

Kuomba: 1 Thes. 5:17-18, "*Ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.*"

Na kumwimbia Mungu sifa, ambayo ilitolewa pasipo kuwa na msaada wa vyombo vya muziki: Efe. 5:19, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.*"

Kitu chochote pungufu au zaidi ya hii haipo kulingana na agizo la mitume.

Kanisa ni jeshi la Bwana

Neno hili linaonyesha kupigana kwa wakati ujao wa kanisa.

Yesu Kristo ndiye Amiri jeshi mkuu. Heb. 2:10, "*Kwa kuwa ilimpasa yeye ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu kwa njia ya mateso.*"

Wakristo wote ni wanajeshi katika jeshi la Bwana.

- 1 Tim. 1:18, "*Mwanangu Timotheo nakukabidhi agizo hilo liwe akiba kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika uvipige vile vita vizuri.*"
- 1 Tim. 6:12, "*Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi.*"
- Efe. 6:10-17, "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi na pepo wabaya katika ulimwengu war oho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama. Basi simameni hali mmejifunga kweli viunoni , na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu;*"

Paulo alimwambia Timotheo katika 2 Tim. 2:3-4, "*Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Yesu Kristo. Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.*"

Hakuna sehemu katika kumhudumia Mungu kwa muoga. Bwana alimwambia Gidioni kuwwarudisha nyumbani majeshi yake yote waliokuwa "*waoga na wenye hofu*" (Waamzi 7:3). Hataivyo ilichukua karibia robo tatu ya jeshi lake, Mungu angekuwa na idadi ndogo ya nafsi majasiri, kuliko kuwa na idadi kubwa iliyojichanganya na waoga.

Mtume Paulo alikuwa mpigaanaji. Hakuwa mtu wa kwenda taratibu. Alipigania hatia yake. Alisema katika Fil. 1:17, "*Bali wengine wanamhubiri Kristo kwa fitina, wala si kwa moyo mweupe wakidhani kuongeza dhiki za kufungwa kwangu.*"

Paulo hakujiuzulu; haakutumia maneno kama, "jiuzulu" au "achia." Alikutana na shetani kila sehemu. Alikutana na wasaliti, ndugu wabaya, waalimu wa uongo; lakini bado alisema, "*Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia habari njema neno la Mungu.*" (Mdo.20:24).

Hivyo, Paulo alipofikia mwisho wa vita ya maisha yake, alifahamu kwa hakika matokeo. 2 Tim. 4:6-8, "*Kwa maana mimi sasa namiminwa,*

na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyovizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake."

Kanisa ni shamba ya mizabibu

Mat. 20:1, "*Kwa maana ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu.*"

Chini ya ishara hii tunaona msemo wa kufanya kazi ya kanisa. Mat. 20:2-16, "*Naye alipokwisha kupatana na wakulima kuwapa kutwa dinari, aliwapeleka katika shamba lake la mizabibu. Akatoka mnamo saa tatu, akaona wengine wamesimama sokoni wasio kuwa na kazi; na hao nao akawaambia enendeni nanyi katika shamba langu la mizabibu, na iliyo haki nitawapa, wakaenda. Akatoka tena mnamo saa sita na saa kenda akafanya vilevile. Hata kama saa kumi na moja akatoka, akakuta wengine wamesimama, akawaambia, mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi? Wakamwambia, kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri. Akawaambia, enendeni nanyi katika shamba langu la mizabibu. Kulipokuchwa, yule bwana wa shamba akamwambia msimamizi wake, waite wakulima uwalipe ujira wao, ukianzia wa mwisho hata wa kwanza. Na walipokuja wale wa saa kumi na moja, walipokea kila mtu dinari. Na wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaidi; na hao pia wakapokea kila mtu dinari. Basi wakiisha kuipokea wakamnung'unikia mwenye nyumba, wakisema hao wa mwisho wamatenda kazi saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi tuliostahimili tabu na hari za mchana kutwa. Naye akamjibu mmoja wao, akamwambia rafiki, sikudhulumu hukupana nami kwa dinari? Chukua iliyo yako uende zako; napenda kumpa huyu wa mwisho sawasawa na wewe. Si halali yangu kutumia vilivyo vyangu kama nipendavyo? Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema? Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho.*"

Katika Mfano wa Bwana wa wafanya kazi katika msitari wa kwanza kabisa ya kifungu hiki tunaona vitu vitatu vimetajwa hapa na Bwana:

Mwenye nyumba alitoka kwenda *"...<u>kuajiri</u> wafanya kazi katika shamba lake la mizabibu..."*

Hakujaribu kuwa ogopesha au kuwalazimisha waingingie katika shamba la mizabibu. Ama Bwana hatamleta mtu katika huduma yake kwa kumthibiti. Anawaita wanaojitoa; hamlazimishi mtu kuingia katika jeshi lake.

Mwenye nyumba alitoka kwenda "*...kuajiri watenda kazi katika shamba lake la mizabibu...*"

Hakuwataka wanaojitenga na wavivu. Hakuna sehemu katika ufalme wa Mungu ya mtu mvivu. Tunapaswa kuwa na "*shauku katika kutenda kazi njema*" (Tito 2:14).

Mwenye nyumba alitoka kwenda "*...kuajiri watenda kazi katika shamba lake la mizabibu...*"

Hivyo, inaleta tofauti mahali ambapo kazi inafanywa; inapaswa kufanywa katika shamba lake la mizabibu.

Yesu alisema katika Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Ni muhimu kiasi gani, basi, ilivyo kuwa katika shamba la mizabibu ya Bwana.

Hitimisho

Sasa, kama unataka kuwa mwenyeji katika ufalme wa Kristo, kiungo katika mwili wake, muumini katika hekalu lake, mwanajeshi katika jeshi lake, na mtenda kazi katika shamba lake la mizabibu, ni lazima uwe katika kanisa lake maana hana raia walioko nje ya ufalme wake, hana kiungo iliyopo nje ya mwili wake, hana waumini walioko nje na hekalu lake. Hana wanajeshi walio nje ya jeshi lake, hana watenda kazi walio nje ya shamba lake la mizabibu.

Kubali wito wake wenye thamani, na katika kuitii injili, uzidishwe kwa rehema katika kanisa lake?

Mtu anawezaje kuwa mshirika katika kanisa lake? Mtu ni lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6, "*Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya

Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend 11:18, *"...Mungu amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani!" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Math. 3:14-17).

Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "imekuwa kwetu **sisi** "*kuitimiza haki yote*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya ubatizo? "kwa ajili ya ondoleo la dhambi." Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile "*Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.*" (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuweka udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama hujafanyika mshiriki katika mwili wa Kristo, kwa nini usizingatie leo?